

Wanafunzi wawili kushiriki maonesho ya sayansi Ireland

Na Lucy Ngowi

WANAFUNZI wawili wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari ya Mzumbe, Morogoro, wamekwenda Dublin, Ireland kushiriki maonesho ya sayansi na teknolojia.

Wanafunzi hao waliondoka jana baada ya kushinda hapa nchini katika ugunduzi walioufanya kuhusu namna ya kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki.

Akizungumza kwenye hafla ya kuwaaga, mwanafunzi mmojawapo, John Method alisema katika ziara hiyo anaamini yeye na mwenzake Edmund Luguku wataifunza mengi

kutoka kwa vijana wenzao ambao wako mbali kiteknolojia ikilinganishwa na hapa nchini.

Method alisema katika ugunduzi walioufanya walibaini kuwa mifuko ya plastiki inasaidia lakini ina madhara makubwa kwa binadamu, kwani katika siku za karibuni imeonekana kuwa wanawake wengi wanafunika vyakula kwa mifuko ya plastiki ambapo kemikali za mifuko hiyo inaingia kwenye chakula hicho na kusababisha saratani.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka katika taasisi ya saratani ya Ocean Road, Dar es Salaam, asilimia 66 ya saratani inayowapata watu inasababishwa na chakula.

"Pia mifuko ya plastiki husababi-

sha vifo kwa mifugo pale wanapokula, huchafua mazingira. Mbu ambao husababisha magonjwa huzaliana kwenye mifuko hiyo kwa sababu haipitishi maji," alisema mwanafunzi huyo.

Naye Meneja wa Taasisi ya Karimjee Jivanjee, Rubama alisema taasisi yao imewatunuku nafasi za masomo wanafunzi hao kwa kuwa washindi wa jumla wa tuzo za wanasayansi chipukizi za Young Scientists Tanzania kwa mwaka 2015.

Katika hafla hiyo ya kuwaaga wanafunzi hao meneja Rubama alisema washindi hao watapata fursa ya kupelekwa masomoni na taasisi hiyo mara baada ya kumaliza elimu ya kidato cha sita.

"Wanafunzi hao watasafiri leo (jana) kuelekea Dublin Ireland ambapo watahudhuria maonesho ya kimataifa ya sayansi na teknolojia ambapo kila mwaka hufanyika mashindano yanayolenga kuhamasisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupenda sayansi," alisema meneja huyo.

Naye mwenyekiti wa heshima wa wa kundi la makampuni ya Karimjee Jivanjee, Hatim Karimjee alisema wamepeva heshima kubwa ya kuweza kuwa sehemu ya tuzo hizo kwani wanaamini kuwa elimu ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Tanzania pia elimu ya sayansi inaweza kuleta fursa nzuri kitaaluma.

Alisema japo mtazamo mkubwa wa taasisi hiyo hivi sasa ni kusaidia taasisi za elimu kwa kuboresha uwezo wake, familia ya Karimjee ilianzisha taasisi mbalimbali za misaada kwenye miaka ya 1950 kabla ya uhuru kwa kujenga shule nyingi, hospitali, zaharani na vituo vya huduma za jamii ikiwemo ukumbi wa Karimjee.

Kwa upande wake Dk Gosbert Kamugisha wa taasisi ya Young Scientists Tanzania (YST), alisema maonesho yaliyofanyika jijini Dar es Salaam yalishirikisha vijana wengi lakini vijana hao wawili ndio walioipata ushindi wa jumla.

Alisema taasisi hiyo inawaweza sha vijana kutanya sayansi kwa vitendo kutoka kwenye nadharia.